# Sala za Wakristo

# Sala za Wakristo

## SALA ZA ASUBUHI NA JIONI,

## MISSA TAKATIFU,

## SAKRAMENTI YA TOBA *Etc.*

*New Edition.*

The Universities' Mission to Central Africa.
ZANZIBAR.
1940.

# Sala za Asubuhi

---

✠ Kwa Jina la Baba na Mwana na Roho Mtakatifu. *Amin.*

Ahidimiwe Utatu Mtakatifu, Mungu Mmoja, sasa na siku zote, na hata milele.

Baba yetu, uliye mbinguni: Jina lako takatifu litukuzwe, Ufalme wako uje, Mapenzi yako yatimizwe, hapa duniani kama huko mbinguni. Utupe leo riziki zetu. Utusamehe makosa yetu, kama sisi tunavyowasamehe waliotukosa. Usitutie majaribuni, lakini utuokoe na maovu. *Amin.*

Salamu, Mariamu, umejaa neema, Bwana yu pamoja nawe; umebarikiwa kuliko wanawake wote; na Yesu, uzao wa tumbo lako, amebarikiwa.

Mariamu Mtakatifu, Mama wa Mungu, utuombee sisi wenye dhambi, sasa, na saa ya kufa kwetu. *Amin.*

*Ukiwa na nafasi, sema,*

Namwamini Mungu Baba Mwenyezi, Muumba mbingu na nchi.

Na Yesu Kristo, Mwana wake pekee, Bwana wetu, Aliyechukuliwa mimba kwa uweza wa Roho Mtakatifu, Akazaliwa na Bikira Mariamu, Akateswa zamani za Pontio Pilato, Akasulibiwa, Akafa, Akazikwa, Akashuka mahali pa wafu; Siku ya tatu akafufuka, Akapaa mbinguni, Ameketi mkono wa kuume wa Mungu Baba Mwenyezi; Kutoka huko atakuja kuwahukumu watu wahai na wafu.

Namwamini Roho Mtakatifu; Kanisa Takatifu, Katholiko; Ushirika wa Watakatifu; Ondoleo la dhambi; Kiyama ya mwili, Na uzima wa milele. *Amin.*

*Sema kila siku,*

**Imani.**

Mungu wangu, nakuamini; nayaamini yote uliyonifundisha katika Kanisa lako, kwa sababu Wewe u Kweli, huwezi kunidanganya.



**Tumaini.**

Mungu wangu, nakutumaini Wewe, ya kuwa utanipa neema na utukufu.

**Upendo**

Mungu wangu, nakupenda, nataka nizidi kukupenda; nimpende na jirani yangu kwa ajili yako.

**Toba**

Mungu wangu, nimesikitika sana kwa kuwa nimekukosa. Kwa msaada wako nataka nisikukose tena.

Mungu Roho Mtakatifu, uwemo moyoni mwangu leo; uniangaze nuru yako; unishirikishe nguvu zako; ili kwa msaada wako nimshinde Shetani na kumpendeza Baba yetu; Kwa Kristo Bwana wetu. *Amin.*

Bwana Yesu, unishike mkono, nisitende dhambi leo.

Mungu Roho Mtakatifu, uniongoze hata nimwone Bwana Yesu uso kwa uso.

✠ Roho za waminifu, kwa rehema ya Mungu, wastarehe katika amani. *Amin.*

## MALAIKA WA BWANA

*Husemwa asubuhi, adhuhuri, na jioni.*

Malaika wa Bwana alimhubiri Mariamu: naye akachukua mimba kwa uweza wa Roho Mtakatifu.

Salamu, Mariamu. *etc.*

Tazama, mimi mjakazi wa Bwana: na iwe kwangu kwa neno lako.

Salamu, Mariamu. *etc.*

Neno alifanyika mwili: akakaa kwetu.

Salamu, Mariamu. *etc.*

*V.* Utuombee Mama Mtakatifu wa Mungu.

*R.* Tustahili kupewa ahadi za Kristo.

Tuombe.

Bwana, tunakusihi, utupe kwa ukarimu neema yako: Ili sisi tuliojua kwa ujumbe wa malaika habari ya kutwaa mwili kwake Yesu Kristo Mwana wako; kwa msalaba na mateso yake tuletwe mpaka utukufu wa ufufuo wake. Kwa Yeye Kristo, Bwana wetu. *Amin.*



¶ *Bali, Wakati wa Pasaka sema kama hivi:—*

Malkia wa mbingu, furahi. Haleluya.

Uliyemchukua tumboni. Haleluya.

Kafufuka kama alivyoahidi. Haleluya.

Kwa Mungu na utuombee. Haleluya.

*V.* Furahi, shangilia, Ee Bikira Mariamu. Haleluya.

*R.* Maana hakika Bwana amefufuka. Haleluya.

Tuombe.

Ee Mungu, umewafurahisha wanadamu wote kwa kufufuka kwake Bwana wetu Yesu Kristo Mwana wako: Tunakuomba tupewe furaha ya uzima wa milele; tukisaidiwa kwa sala za Bikira Mariamu aliyemzaa. Kwa Yeye, Kristo Bwana wetu. Amin.

# Sala za Jioni.

✠ Kwa Jina la Baba na Mwana na Roho Mtakatifu. *Amin.*

Baba yetu.

Salamu, Mariamu.

Namwamini.

Mungu wangu, nakushukuru sana kwa kuwa umenilinda leo mchana. Unilinde, nakusihi, usiku huu nisitende dhambi, Shetani asinidhuru.

Utukufu.

*Sasa umwombe Roho Mtakatifu akusaidie upate kuyafahamu makosa yako.*

Mungu Roho Mtakatifu, unisaidie nipate kuyafahamu makosa yangu yote niliyotenda leo.

*Sasa fikiri sana upate kukumbuka matendo yako yote tangu ulipoamka asubuhi, na jinsi ulivyokosa leo. Hivi:*

Nimewaza mabaya gani?

Nimesema mabaya gani?



Nimetenda mabaya gani?

Nimeacha vipi vilivyonipasa kufanya leo?

*Kisha sema:*

Naungama kwa Mwenyezi Mungu, na kwa Watakatifu wote, ya kwamba nimekosa sana, kwa mawazo, na maneno, na matendo; kwa kosa langu, kosa langu, kosa langu baya sana (*hapa taja makosa yako*). Kwa hiyo nawasihi Watakatifu wote waniombee kwa Bwana Mungu wetu.

Mwenyezi Mungu anirehemu, anisamehe makosa yangu, anifikishe kwenye uzima wa milele. Amin.

Bwana Yesu Kristo, kwa ajili ya dhambi zangu uliinyosha mikono yako msalabani: univute kwako, ninakusihi, ili nisiingie katika dhambi. Unijalie nizitubie dhambi zangu kwa moyo, na kujiepusha nazo; nizidi kukupenda na kukutii leo na siku zote, kwa rehema zako. Amin.

Baba Mwenyezi, uwabariki wa nyumba yangu na wote nilio nao ; uwabariki wazee wangu, ndugu zangu...., jamaa zangu......, rafiki zangu...... Uwaagize Malaika zako watakatifu watulinde sote, utuhifadhi usiku huu na siku zote. Kwa Kristo Bwana wetu. Amin.

Uwabariki, Baba, Wakristo wote, kila mtu kwa haja yake. Uwasaidie walio kufani. Kwa Kristo Bwana wetu. Amin.

*Jitakie maombezi ya Mtakatifu wako.*

*Fulani* Mtakatifu, uniombee.

✠ Roho za waminifu, kwa rehema ya Mungu, wastarehe katika amani. Amin.

*Ukijilaza kitandani, sema :*

✠ Kwa Jina la Baba na Mwana na Roho Mtakatifu. Amin.

Bwana Yesu, unishike mkono nisitende dhambi. Amin.

# Sala za Mtu na Mkewe.

*Yafaa sala hizi zitangulie ; zikiisha, kila mmoja amalize sala zake za siri. Ni wajibu wa Mkristo kuwasalisha wa nyumbani mwake kila siku.*

## ASUBUHI.

*Wote wawili wapige magoti pamoja. Kama wapo watoto wapige magoti nao.*

✠ Kwa Jina la Baba na Mwana na Roho Mtakatifu. *Amin.*

Baba yetu.

Salamu, Mariamu.

Namwamini,

Tuombe.

Mwenyezi Mungu. Baba yetu.<br>
Twakushukuru sana kwa kutulinda na hatari zote za usiku huu.<br>
Za mwili na za roho.<br>
Na kwa mibaraka yote tunayopewa nawe.<br>
Utusamehe kila tulilokukosa ;<br>
Utupe moyo wa toba ;<br>
Kwa Kristo Bwana wetu. *Amin.*

Mwenyezi Mungu utubariki sisi na nyumba yetu.

Uwabariki na jamaa zetu.

Wasiokujua uwaongoe,

Waliokosa uwajalie toba.

Waliofariki uwarehemu.

Umbariki Askofu wetu, na makasisi wetu.

Utulinde na dhambi.

Bwana Yesu, utuvute kwako,

Sisi tunaokumbuka jeraha zako,

Tusitende dhambi leo.

Roho Mtakatifu, utuongoze katika njia njema. *Amin.*

✠ Roho za waminifu, kwa rehema ya Mungu, wastarehe katika amani. *Amin.*



## JIONI.

*Wote wawili wapige magoti pamoja*
*Kama wapo watoto wapige magoti nao.*

✠ Kwa Jina la Baba na Mwana na Roho Mtakatifu. *Amin.*

Baba yetu

Salamu, Mariamu.

Namwamini.

Mwenyezi Mungu twakushukuru kwa rehema zako za mchana huu.

Utukufu.

Twaungama kwa Mwenyezi Mungu,
Na kwa Watakatifu wote,
Ya kwamba tumekosa sana.
Kwa mawazo, na maneno, na matendo;
Kwa kosa letu, kosa letu, kosa letu baya sana.

Kwa hiyo twawasihi Watakatifu wote
Watuombee kwa Bwana Mungu wetu.

Mwenyezi Mungu aturehemu, atusamehe makosa yetu,
Atufikishe kwenye uzima wa milele. *Amin.*
Uingie, Bwana, twakusihi, katika nyumba hii,
Uondolee mbali hila zote za adui.
Malaika zako watakatifu wakae humo watulinde katika amani.
Baraka yako itukalie daima ;
Kwa Kristo Bwana wetu. *Amin.*

✠ Roho za waminifu kwa rehema ya Mungu wastarehe katika amani. *Amin.*

*Wajitakie maombezi ya Watakatifu wao,*
*Fulani* Mtakatifu, utuombee.
*Fulani* Mtakatifu, utuombee.

# Missa Takatifu.

---

## UKIUTAKA USHIRIKA MTAKATIFU.

*Sema sala hizi usiku, kabla hujalala. na tena Kanisani kabla ya Missa.*

✠ Kwa Jina la Baba na Mwana na Roho Mtakatifu. *Amin.*

Baba yetu.

Salamu, Mariamu.

Mwenyezi Mungu, ninakuja kwako kwa sababu umeniita :
Ninakuja niitoe sadaka mbele yako :
Ninakuja nimpokee Kristo, Mwana wako.
Ninakuomba unipe Roho yako Mtakatifu sasa anifanye tayari kumpokea Yesu.
Mwenyezi Mungu sistahili kumpokea Kristo Yesu, Mwili wake na Damu yake :
Maana nimetenda dhambi ; mchafu mimi machoni pako.

Ninakuomba unisamehe dhambi zangu zote: kwa Kristo Bwana wetu. *Amin.*

Bwana Yesu, ninakuja kwako, kwa rehema yako.

Bwana Yesu, unisamehe dhambi zangu zote.

Bwana Yesu, unitakase uchafu wangu.

Bwana Yesu, unijaze nguvu zako na neema zako.

Uje kwangu, Bwana Yesu, ukae ndani yangu.

Uje kwangu, Bwana Yesu, usiniache tena.

Uje kwangu, Bwana Yesu, unitawale daima.

Kwa Mwili wako unipe nguvu.

Kwa Damu yako unisafishe.

Bwana Yesu, nakupenda.

Bwana Yesu, nataka nizidi kukupenda.

Bwana Yesu, ninaomba nikupendeze na kukutii hata mwisho. *Amin.*

---



## USIPOTAKA KUSHIRIKI.

*Ufikapo Kanisani, sema,*

✠ Kwa Jina la Baba na Mwana na Roho Mtakatifu. *Amin.*

Mungu wangu, umeniita nije leo kukutolea sadaka hii.

Nakushukuru sana. Nisaidie nikutolee sadaka hii inipasavyo, kwa heshima na shukrani kuu.

Uikubali sadaka hii kwa utukufu wako:

Uikubali sadaka hii, nikushukuru kwa yote uliyonitendea na kunipa:

Uikubali sadaka hii, unipe ondoleo la dhambi:

Uikubali sadaka hii, unipatie yote unayoyajua kuwa nayahitaji, kwa roho na kwa mwili.

Uikubali sadaka hii, kwa ajili ya wahai na wafu, wapewe masamaha na baraka.

Unijalie nizidi kujitoa nafsi yangu, roho yangu na mwili wangu, kuwa sadaka ya kukupendeza.

Kwa rehema zako umbariki Kasisi atakayeitoa Missa hii, na watu wote watakaoihudhuria. *Amin.*

---

## KUNYUNYIZIWA MAJI YA BARAKA.

*Simama, Fumba mikono.*

*Ant.* Unisafishe, Ee Bwana kwa husopo, nami nitakuwa safi: unioshe, nami nitakuwa mweupe kuliko theluji.

*Zab.* Unirehemu Ee Mungu: kwa kadiri ya fadhili zako.

Utukufu.

*Ant.* Unisafishe, *etc.*

*V.* Ee Bwana, utuonyeshe rehema zako.

*R.* Utupe wokofu wako.

*V.* Ee Bwana, usikie kuomba kwangu.

*R.* Kilio changu kikufikie.

*V.* Bwana akae nanyi.

*R.* Akae na roho yako.

Tuombe.

Utusikie, Bwana Mtakatifu, Baba Mwenyezi, Mungu wa milele: Ukubali ku-



mtuma Malaika wako mtakatifu kutoka mbinguni awajie wote wakaao nyumbani humu; awahifadhi, awaburudishe, awaponye na kuwalinda. Kwa Kristo Bwana wetu. *Amin.*

¶ *Wakati wa Pasaka.*

*Ant.* Naliona maji yakitoka hekaluni upande wa kuume, Haleluya: na wote waliofikiwa na maji hayo wakaokoka; nao husema, Haleluya, Haleluya.

*Zab.* Mshukuruni Bwana kwa kuwa yu mwema: kwa maana fadhili zake ni za milele.

Utukufu.

*Ant.* Naliona maji, *etc.*

*V.* Ee Bwana, utuonyeshe rehema zako. Haleluya.

*R.* Utupe wokofu wako. Haleluya.

*V.* Ee Bwana, usikie kuomba kwangu.

*R.* Kilio changu kikufikie.

*V.* Bwana akae nanyi.

*R.* Akae na roho yako.

Tuombe.

Utusikie Bwana Mtakatifu, Baba Mwenyezi, Mungu wa milele: Ukubali kumtuma Malaika wako mtakatifu kutoka mbinguni awajie wote wakaao nyumbani humu; awahifadhi, awaburudishe, awaponye na kuwalinda. Kwa Kristo Bwana wetu. *Amin.*

## MISSA TAKATIFU

*Ukipiga magoti, au kusimama, huna kitabu, fumba mikono, fumba macho. Amri zifuatazo juu ya kusimama na kupiga magoti yafaa wakati wa kuimba Missa.*


*Piga magoti.*

¶ *Kasisi aseme*


✠ Kwa Jina la Baba na Mwana na Roho Mtakatifu. *Amin.*

*V.* Nitakwenda madhabahuni kwa Mungu.

*R.* Kwa Mungu aliye furaha yangu na shangwe yangu.



Kasisi anajiweka tayari kwa Missa.



Kasisi anasema Maungamo.



*Zab.* 43.

(*Katika Missa ya wafu Zaburi isisemwe*).

1. Unihukumu, Bwana, unitetee kwa taifa lisilo haki : uniokoe na mtu wa hila, asio haki.

2. Kwa kuwa Wewe ndiwe Mungu wa nguvu zangu ; kwa nini umenifukuza : kwa nini ninakwenda nikihuzunika, adui wakinionea ?

3. Niletewe nuru yako na kweli yako, ziniongoze : zinifikishe kwenye mlima wako mtakatifu na hata masikani zako.

4. Hivyo nitakwenda madhabahuni kwa Mungu, kwa Mungu aliye furaha yangu na shangwe yangu : nitakusifu kwa kinubi, Mungu, Mungu wangu.

5. Ya nini umeinama, roho yangu : na kufadhaika ndani yangu ?

6. Umtumaini Mungu, kwa maana nitakuja kumsifu : aliye afya ya uso wangu na Mungu wangu.

Utukufu.

*V.* Nitakwenda madhabahuni kwa Mungu
*R.* Kwa Mungu aliye furaha yangu na shangwe yangu.
*V.* ✠ Msaada wetu u katika Jina la Bwana.
*R.* Aliyezifanya mbingu na nchi.

¶ *Kasisi aseme*

Naungama kwa Mwenyezi Mungu *etc.*

¶ *Kisha watu wote waseme.*

Mwenyezi Mungu akurehemu, akusamehe makosa yako, akufikishe kwenye uzima wa milele. *Amin.*

¶ *Watu wote waseme.*

Naungama kwa Mwenyezi Mungu, kwa Watakatifu wote, na kwako, baba, ya kwamba nimekosa sana, kwa mawazo, na maneno, na matendo; kwa kosa langu, kosa langu, kosa langu baya sana. Kwa hiyo nawasihi Watakatifu wote waniombee, na wewe, baba, uniombee kwa Bwana Mungu wetu.



¶ *Kisha Kasisi aseme,*

Mwenyezi Mungu akurehemuni, akusameheni makosa yenu, akufikisheni kwenye uzima wa milele. *Amin.*

Bwana Mwenyezi na mwenye rehema atujalie masamaha, ✠ ghofira, na ondoleo la dhambi zetu. *Amin.*

*V.* Urudi, Ee Mungu, utuhuishe.
*R.* Watu wako wakufurahie.
*V.* Ee Bwana utuonyeshe rehema zako.
*R.* Utupe wokofu wako.
*V.* Ee Bwana, usikie kuomba kwangu.
*R.* Kilio changu kikufikie.
*V.* Bwana akae nanyi.
*R.* Akae na roho yako.

Tuombe.

Mwenyezi Mungu, kwako Wewe mioyo yote i wazi, haja zote zimejuliwa, wala hakuna la siri usilolijua: Uyasafishe mawazo ya mioyo yetu kwa kutupuzia Roho

yako Mtakatifu; ili tukupende hasa, na kuliadhimisha Jina lako takatifu kama itupasavyo. Kwa Kristo Bwana wetu. *Amin.*


*Simama.*

## INTROIT.


Bwana, uturehemu. (iij)
Kristo, uturehemu. (iij)
Bwana, uturehemu. (iij)

UTUKUFU una Mungu juu, katika nchi amani kwa watu aliowaridhia. Twakusifu, twakuhimidi, twakuabudu, twakutukuza, twakushukuru kwa ajili ya utukufu wako mkuu, Bwana Mungu, Mfalme wa mbinguni, Mungu Baba Mwenyezi.

Bwana Mwana pekee, Yesu Kristo: Bwana Mungu, Mwana Kondoo wa Mungu, Mwana wa Baba: Uzichukuaye dhambi za ulimwengu, uturehemu. Uzichukuaye dhambi za ulimwengu, ukubali kuomba kwetu. Uketiye mkono wa kuume wa Mungu Baba, uturehemu.



Kasisi anasoma Waraka.



Kasisi anasoma Injili.



Kwa kuwa ndiwe uliye peke yako Mtakatifu; ndiwe peke yako Bwana; ndiwe peke yako uliye juu, Yesu Kristo, pamoja na ✠ Roho Mtakatifu, katika utukufu wake Mungu Baba. *Amin.*

*Simama vile vile,*

*V.* Bwana akae nanyi.

*R.* Akae na roho yako.

[*Askofu aseme,*

*V.* Amani kwenu.

*R.* Ikae na roho yako].

Tuombe.

SALA.

*Keti.*

SOMO.

*R.* Tumshukuru Mungu (*isiimbwe*).

*Simama.*

GRADUALE.

*V.* Bwana akae nanyi.

*R.* Akae na roho yako.

*V*. Sehemu ya Injili takatifu, kama ilivyoandikwa na *N*. Mtakatifu.

*Umwonapo Kasisi anajitia msalaba pajini, sema moyoni mwako.*

Bwana ✠ unibariki : Bwana awe ✠ moyoni mwangu na midomoni ✠ mwangu. Amin.

*Kisha itika,*

*R*. Atukuzwe Bwana.

INJILI.

*R*. Asifiwe Kristo. (*Isemwe tu*).

*Keti.*

HOTUBA.

*Simama.*

*Kuwaruhusu wasio na amani.*

Wanafunzi mwombeni Bwana.

Sisi tuaminio tuwaombee Wanafunzi wote wa Kanisa Katholiko.

*V*. Ee Bwana, uwafundishe elimu ya haki.

*R*. Bwana, uwarehemu.



*V*. Uwafunulie Injili ya kweli.

*R*. Bwana, uwarehemu.

*V*. Uwaunganishe na Kanisa lako Takatifu, Katholiko, Apostoliko.

*R*. Bwana, uwarehemu.

*V*. Ee Bwana uwalinde na mabaya yote.

*R*. Bwana, uwarehemu.

Tuombe.

Bwana, Mungu wetu, uliyempeleka Mwana wako pekee, Yesu Kristo, awe wokofu wa wanadamu wote: Tunakuomba uwaangalie watumishi wako, wanafunzi wake, uwape Ubatizo Utakatifu kwa wakati wako; ili hawa, pamoja na sisi, walitukuze Jina lako takatifu la Baba na Mwana na Roho Mtakatifu, sasa na siku zote na hata milele na milele. *Amin.*

Wanafunzi wa Kristo, nendeni zenu.

Wenye kitubio cha Kanisa, ombeni.

Sisi nasi tuwaombee hawa ndugu zetu wenye kitubio.

Tuombe.

Mungu Mwenyezi wa milele, Baba wa mbinguni : Tunakuomba uwatazame watu hawa wanaokurudia, kama yule mwana mpotevu alivyomrudia baba yake, akakubaliwa naye kwa kuwa alitubu : uwakubali, uwarudishe katika Kanisa lako takatifu, wenye hali ya sifa na heshima. Kwa Kristo Bwana wetu. *Amin.*

Wenye kitubio cha Kanisa, nendeni zenu.

---

NAMWAMINI Mungu mmoja, Baba Mwenyezi, Muumba mbingu na nchi, Na vitu vyote vinavyoonekana na visivyoonekana.

Na Bwana mmoja Yesu Kristo, Mwana pekee wa Mungu, Mwana wa azali wa Baba. Yu Mungu anatoka katika Mungu, Yu Nuru anatoka katika Nuru, Yu Mungu kweli anatoka katika Mungu kweli, Mwana wa azali asiyeumbwa,



Mwenye Uungu mmoja na Baba, Kwa Yeye huyu vitu vyote vyaliumbwa. Alieshuka kutoka mbinguni, kwa ajili yetu wanadamu, na kwa wokofu wetu. (*Piga magoti*) **Akatwaa mwili kwa uweza wa Roho Mtakatifu katika Bikira Mariamu, Akawa mwana Adamu,** (*Simama*). Akasulibiwa kwa ajili yetu, zamani za Pontio Pilato. Aliteswa, akazikwa. Siku ya tatu akafufuka kama yanenavyo Maandiko matakatifu, Akapaa mbinguni, Ameketi mkono wa kuume wa Baba. Naye atakuja tena kwa utukufu kuwahukumu watu wahai na wafu ; Na milki yake haina mwisho.

Namwamini Roho Mtakatifu, Bwana, Mtoa uzima, Atokaye katika Baba na Mwana, Anayeabudiwa na kutukuzwa pamoja na Baba na Mwana, Aliyenena kwa vinywa vya Manabii. Naamini Kanisa Moja, Takatifu, Katholiko, na Apostoliko. Nakiri Ubatizo Mmoja wa kuondolea dhambi. Natazamia Kiyama ya wafu, na ✠ Uzima wa ulimwengu ujao. Amin.

*V.* Bwana akae nanyi.
*R.* Akae na roho yako.


## OFFERTORIO.

*Toa Sadaka zako mfukoni.*
(*Kasisi anasema kwa siri*)


Baba Mtakatifu, Mungu Mwenyezi, wa milele, uikubali sadaka hii safi, ambayo mimi mtumishi wako, nisiyestahili, ninakutolea, Ee Mungu wangu uliye hai, wa kweli, kwa ajili ya dhambi na makosa yetu yasiyohesabika; na kwa ajili ya wote wanaohudhuria, na kwa ajili ya Wakristo waminifu wote, wahai na wafu; itupatie wokofu, na mwisho wake, uzima wa milele. Amin.

Mungu uliuumba utu wetu mtakatifu kwa jinsi ya ajabu, ukaufanya upya kwa ajabu izidiyo; utujalie, kwa njia ya siri hii ya maji na divai, tushirikishwe Uungu wake asiyekataa kuushiriki utu wetu, Yesu Kristo Mwana wako, Bwana wetu: Aishiye na kumiliki pamoja nawe, katika umoja wa Roho Mtakatifu, Mungu, daima, milele na milele. Amin.

Tunakutolea, Bwana, kikombe hiki cha wokofu tukikuomba, kwa rehema yako, kipandishwe mbele yako mbinguni, kiwe na kibali machoni pako, kwa ajili ya wokofu wetu sisi na wa ulimwengu pia. Amin,



Offertorio.


Kasisi ananawa mikono yake.



Tukinyenyekea kwako, Baba na kuleta majuto ya moyoni, tukubaliwe nawe: sadaka yetu itolewe vizuri leo mbele yako, ili ikupendeze Wewe, Bwana Mungu.

Mungu Mwenyezi wa milele, ututakasaye uje: uibariki sadaka hii iliyowekwa tayari kwa utukufu wa Jina lako.

[*Kasisi anaponawa asoma Zaburi*]

Utatu Mtakatifu, uikubali sadaka hii tuitoayo kwako, tukimkumbuka Bwana wetu Yesu Kristo, alivyoteswa na kufufuka na kupaa mbinguni: nasi tunakuomba Watakatifu wako walioko mbinguni watuombee sisi tuwakumbukao hapa duniani. Kwa Kristo Bwana wetu. Amin.

## *Piga magoti.*

## *Kasisi aseme kwa sauti kubwa.*

Ombeni, ndugu, sadaka yangu na yenu iwe na kibali kwa Mungu, Baba Mwenyezi.

*R.* Bwana aikubali hii sadaka mikononi mwako, kwa sifa na utukufu wa Jina lake, kwa faida yetu, na kwa faida ya Kanisa lake Takatifu pia. (*Kasisi aseme*, Amin.)

*Hufuata* **Sala za Siri.** *Zikiisha Kasisi apaaze sauti, aseme, au kuimba,*

Daima, milele na milele.

*R.* Amin.

*V.* Bwana akae nanyi.

*R.* Akae na roho yako.

*V.* Inueni mioyo.

*R.* Twaiinua kwa Bwana.

*V.* Na tumshukuru Bwana Mungu wetu.

*R.* Ina haki, tena ni wajibu.

Ndiyo wajibu wetu, ina haki, tena ya faradhi kwetu, kila wakati na kila mahali, tukushukuru Bwana Mtakatifu, Baba Mwenyezi, Mungu wa milele.*

* *Ikiwa ni Siku Kun kubwa, maneno yafuatayo hubadilika.*

Kwa Kristo Bwana wetu.

Kwa yeye, sisi nasi, pamoja na Malaika na Malaika wakuu, na jeshi la mbinguni lote pia, twakutukuza na kuliadhimisha Jina lako tukufu; tukikusifu daima tukisema,

Mtakatifu........(*Taz. uk* 40).



¶ *Dibaji ya Siku Kuu ya Utatu na Siku za Bwana zisizowekewa Dibaji.*

Ndiyo wajibu wetu, ina haki, tena ya faradhi kwetu, kila wakati na kila mahali, tukushukuru, Bwana Mtakatifu, Baba Mwenyezi, Mungu wa milele.


Wewe, pamoja na Mwana wako pekee na Roho Mtakatifu, U Mungu mmoja, Bwana mmoja : umoja wako si mithili ya nafsi iliyo moja, bali ni Utatu wa Uungu mmoja. Kwa maana yote tuyaaminio juu ya utukufu wako tuliofunuliwa, ndiyo tuyaonayo juu ya Mwana wako, na juu ya Roho Mtakatifu, tusitie tofauti wala kupambanua. Hata tuukiripo Uungu wa kweli, wa milele, huabudika tofauti za nafsi, na umoja wa Uungu, na utukufu sawa sawa.

Ndizo waziabuduzo Malaika na Malaika Wakuu, Makerubi nao, na Maserafi, ambao kila siku, kwa sauti moja, wanakuimbia, hawaachi, wakisema.

MTAKATIFU, Mtakatifu, Mtakatifu, Bwana Mungu wa majeshi, mbingu na nchi zimejaa utukufu wako : Utukufu una Wewe Bwana uliye juu.

✠ Ndiye mbarikiwa ajaye kwa Jina la Bwana. Hosana uliye juu.


*Simama. Fumba mikono.*




**Sala ya Kanuni.**

Mwenyezi Mungu wa milele, tunakusihi uzipokee sadaka hizi zetu, pamoja na sala zetu.

Tunakuomba ulipulizie Kanisa lako Katholiko roho ya kweli na ya kupatana.



Mtakatifu, Mtakatifu Mtakatifu.

*Ukumbusho wa Wahai.*

Umlinde Mfalme wetu, *N.*; utujalie tutawaliwe chini yake kama vile upendavyo Wewe.

Baba wa mbinguni, umbariki Askofu wetu *N.*; uwabariki na Maaskofu wote, na wote wachungao roho za watu, walihubiri neno lako kwa mafundisho yao na kwa mwenendo wao safi.

Uwape neema watu wako wote, wakutumikie kwa kweli siku zao zote.

Tena uwasaidie walio na taabu, huzuni, ugonjwa, au haja nyingineyo yote, hasa *N.* na *N.*

Tunakuomba utubariki na sisi tuliopo hapa, tunafanya ukumbusho wa kufa kutukufu kwa Mwana wako, Kristo Bwana wetu. *Amin.*

*Ukumbusho wa Watakatifu.*

Nasi tunakushukuru sana kwa kuwa umetuonyesha uweza wa neema yako katika Watakatifu wako wote ; zaidi katika Mariamu Bikira mbarikiwa mtukufu,



Mama wa Mwana wako Yesu Kristo, Bwana wetu na Mungu wetu ; na katika Babu Watakatifu, katika Manabii, Mitume na Mashahidi.

Tunakuomba, Bwana, tuwafuatishe hawo, imani yao na utii wao, kwa Kristo Bwana wetu. *Amin.*

*Ukumbusho wa Wafu.*

Tena Bwana, tunawatakia rehema watumishi wako wote waliofariki dunia katika imani ; hasa *N.* na *N.*; uwajalie, tunakusihi, rehema yako na amani ya milele, ukawafikishe pamoja na sisi, siku ya kiyama, kunako utukufu wa Mwana wako.

Utujalie haya, Baba, kwa ajili yake Yeye, Yesu Kristo, Msuluhisha na Mwombezi wetu. *Amin.*

*Ukumbusho wa Kufa kwa Bwana.*

Ee Mungu, Baba wa mbinguni, kwa wema na huruma zako ulitupa Mwana wako pekee, Yesu Kristo, afe katika msalaba kwa ukombozi wetu, naye alijitoa nafsi yake kuwa sadaka isiyo mfano, awe


dhabihu timilifu, sadaka kamili, na kafara ya kutosha, kwa ajili ya dhambi za ulimwengu wote. *Piga Magoti.* Ameliamuru kumbukumbu la kufa kwake kwa thamani, na, katika Injili yake takatifu, ametuusia tulifulize daima hata atakaporudi.

### *Kuutaka Uweza wa Roho Mt.*

Utusikie, tunakuomba, Ee Baba wa rehema, uvibariki viumbe hivi vyako, mkate na divai, na kuvitakasa kwa Roho yako Mtakatifu na kwa Neno lako, viwe kwetu Mwili wa thamani wa Mwana wako Yesu Kristo, na Damu yake.

### *Kufanya Wakf.*

Yeye usiku ule ule aliotolewa alitwaa mkate, akainua macho yake kwako, Mungu Baba Mwenyezi, akashukuru, akaubariki, akaumega, akawapa wanafunzi wake, akisema, Twaeni. mle, HUU NDIO MWILI WANGU ULIOTOLEWA KWA AJILI YENU. Fanyeni hivi kwa ukumbusho wangu.



Kuweka Wakfu Mkate



Kuweka Wakfu Divai



Na vivi hivi baada ya kula, akakitwaa kikombe, akashukuru, akakibariki, akawapa wanafunzi wake, akisema, Nyweeni nyote hiki; kwa maana HII NDIYO DAMU YANGU YA AGANO JIPYA, IMWAGIKAYO KWA AJILI YENU NA KWA WATU WENGI ILI IWE ONDOLEO LA DHAMBI. Fanyeni hivi, kila mtakapokunywa, kwa ukumbusho wangu. *Amin.*

### *Kuitaja Sadaka.*

Kwa hiyo, Ee Bwana, Baba wa mbinguni, sisi watumishi wako tunatoa Sadaka kwako, uliye peke yako Mtukufu, ndiyo vitu vyako ulivyotupa, Sadaka hii safi, Sadaka takatifu, Sadaka isiyo mawaa, Mkate wa uzima wa milele, na Kikombe cha wokofu wa daima; tukikukumbuka Kuteswa kutakatifu kwa huyu, Kristo, Mwana wako Bwana wetu, na Kufufuka kwake kwa uweza, na Kupaa kwake kutukufu; na kukushukuru kwa mema yote kuliyotupatia. *Amin.*

*Kuliombea Kanisa zima.*

Tunakuomba, Baba uliye mwema, uikubali Sadaka hii yetu ikutukuzayo na kukushukuru ; utujalie sisi, pamoja na Kanisa lako pia, masamaha ya dhambi zetu, na mema yote yaliyopatikana kwa mateso ya Mwana wako mpendwa.

*Kuwaombea Washiriki.*

Nasi, Ee, Bwana, tunajitoa sadaka kwako, nafsi zetu, roho zetu, na miili yetu. Tunakuomba ye yote atakayevipokea vitakatifu hivi aushiriki vema Mwili wa thamani wa Mwana wako Yesu Kristo na Damu yake, ajazwe neema na baraka yako ya mbinguni, na kufanywa mwili mmoja naye. *Amin.*

*Sisi na Kristo.*

Nasi tusiostahili tunakuomba, Ee Baba, uamuru Sadaka hii yetu ichukuliwe na Malaika wako mtakatifu, pamoja na sala zetu, kunako madhabahu ya juu, mbele yako Mungu uliye Mtukufu, kwa Kristo Bwana wetu.



Kwa Yeye, pamoja na Yeye, na ndani yake Yeye, iwe kwako Mungu Baba Mwenyezi, katika umoja wa Roho Mtakatifu, heshima yote na utukufu, daima, milele na milele. *Amin.*

Tuombe.

*Simama. Fumba mikono.*

Kama vile Mwokozi wetu Kristo alivyotuagiza, akatufundisha, tunathubutu kusema,

Baba yetu, uliye mbinguni : Jina lako takatifu litukuzwe, Ufalme wako uje, Mapenzi yako yatimizwe, hapa duniani kama huko mbinguni. Utupe leo riziki zetu. Utusamehe makosa yetu, kama sisi tunavyowasamehe waliotukosa. Usitutie majaribuni, lakini utuokoe na maovu. Amin.

*Piga magoti.*

Utuokoe, tunakuomba, Ee Bwana, na maovu yote. Ukubali maombezi atuombeayo Mariamu Bikira wa daima,

Mama wa Mungu, pamoja na mitume wako wabarikiwa, na Watakatifu wako wote; utupe amani siku zetu; utusaidie kwa rehema zako, tukae mbali na dhambi siku zote, wala tusifadhaike kwa neno lo lote. Kwa Yeye, Bwana wetu, Yesu Kristo, Mwana wako; Aishiye na kumiliki pamoja nawe, katika umoja wa Roho Mtakatifu, Mungu,

*V.* Daima, milele na milele.

*R.* Amin.

*V.* Amani ya Bwana ikae nanyi daima.

*R.* Ikae na roho yako.

(*Kasisi aseme kwa siri*).

Kristo ametolewa kwa ajili yetu, Mwana Kondoo wetu wa Pasaka, tokea alipozichukua dhambi zetu mwilini mwake katika Msalaba; kwa kuwa Yeye ndiye Mwana Kondoo wa Mungu, azichukuaye dhambi za ulimwengu; kwa hiyo tuishiriki karamu ya Bwana kwa mioyo safi, yenye furaha.



Mwana Kondoo wa Mungu, uzichukuaye dhambi za ulimwengu, Uturehemu.

Mwana Kondoo wa Mungu, uzichukuaye dhambi za ulimwengu, Uturehemu.

Mwana Kondoo wa Mungu, uzichukuaye dhambi za ulimwengu, Utupe amani yako.

*Katika Missa ya Wafu.*

Mwana Kondoo wa Mungu, uzichukuaye dhambi za ulimwengu, Uwape raha.

Mwana Kondoo wa Mungu, uzichukuaye dhambi za ulimwengu, Uwape raha.

Mwana Kondoo wa Mungu, uzichukuaye dhambi za ulimwengu, Uwape raha ya milele

*Katika kurasa* 52 *hata* 59 *zifuatazo,* **52, 54, 56, 58,** *zinahusu watakao kushiriki*: **53, 55, 59,** *zinahusu wasiotaka kushiriki.*

UKITAKA KUSHIRIKI

*Ukiisha imba Mwana Kondoo, au Kasisi akiisoma, sema moyoni sala hizi kabla hujaenda madhabahuni :*

Bwana Yesu, ninakuomba uje kwangu, unisafishe.

Bwana Yesu, uje kwangu, uniponye roho yangu.

Bwana Yesu, uje kwangu, unipe nguvu zako.

Bwana Yesu, nakupenda. Uje kwangu, ukae ndani yangu.

Yesu, Bwana wangu na Mungu wangu, uje kwangu; ukae ndani yangu.

*Sema pamoja na wenzako.*

Bwana, sistahili kuikaribia hii meza yako. Ninakuomba unijalie niile Nyama ya Mwana wako mpendwa Yesu Kristo, na kuinywa Damu yako, ili mwili wangu wenye dhambi usafishwe kwa Mwili wake, na roho yangu kwa Damu yake ya thamani. Kwa Yeye, Kristo Bwana wetu. Amin.



USIPOTAKA KUSHIRIKI

(1) *Baada ya kuimbwa, au kusomwa,* Mwana Kondoo, *sema, mara mbili tatu, moyoni.*

Bwana Yesu, Mungu wangu, Mwokozi wangu, nakupenda : unijalie nizidi kukupenda.

Bwana Yesu, Mungu wangu, Mfalme wangu, nakuamini : unijalie nizidi kukuamini.

Bwana Yesu, Mungu wangu, Bwana wangu, ninajiweka kwako unijalie nikutii hata kufa.

Bwana Yesu, sikupokei leo katika Sakramenti, lakini uje, ukae ndani yangu.

Uje, Bwana Yesu, ukae ndani yangu.

(2) *Washiriki wasemapo sala yao na kuungama, usiwasikilize. Bali, sema sala hii.*

Mungu Baba, uikubali Sadaka hii yangu, Sadaka ya Mwana wako Yesu Kristo, Bwana wangu na Mwokozi wangu.

UKITAKA KUSHIRIKI

Naungama kwa Mwenyezi Mungu, kwa Watakatifu wote, na kwako, baba, ya kwamba nimekosa sana, kwa mawazo, na maneno, na matendo; kwa kosa langu, kosa langu, kosa langu baya sana. Kwa hiyo nawasihi Watakatifu wote waniombee, na wewe, baba, uniombee kwa Bwana Mungu wetu.

*Kasisi atakujibu : wewe umsikilize vema.*

Mwenyezi Mungu akurehemuni, akusameheni makosa yenu, akufikisheni kwenye uzima wa milele. *Amin.*

Bwana Mwenyezi na mwenye rehema akujalieni masamaha, ✠ ghofira. na ondoleo la dhambi zenu. *Amin.*

Huyu ndiye Mwana Kondoo wa Mungu, azichukuaye dhambi za ulimwengu.

Bwana, si stahili yangu Wewe uingie chini ya dari yangu; lakini sema neno tu, na roho yangu itapona



USIPOTAKA KUSHIRIKI

Nakupa Sadaka hii, ikupendeze.

Nakupa Sadaka hii, ikutukuze.

Nakupa Sadaka hii, inipatie haja zangu za haki.

Baba, kwa ajili yake, unibariki roho na mwili.

Unijalie nifanye mapenzi yako. uwabariki wote wa nyumbani mwangu.

Uwabariki jamaa zangu na rafiki zangu.

Umbariki askofu wangu.

Uwabariki Makasisi wangu na walimu wangu.

Uwabariki watu wote wa Kanisa lako.

Utubishe wenye dhambi.

Uvute wasio wakristo.

Ufanye imara walio waaminifu.

Ufundishe wanafunzi na wasikiaji.

Uulete ufalme wako duniani.

Uwape amani waliofariki katika dunia.

Baba : unisikie, kwa ajili ya Sadaka

**UKITAKA KUSHIRIKI**

*Wewe jibu pamoja na wenzako,*

Bwana, si stahili yangu Wewe uingie chini ya dari yangu; lakini sema neno tu, na roho yangu itapona.

*Kasisi atajibu, wewe umsikilize vema.*

Bwana, si stahili yangu Wewe uingie chini ya dari yangu; lakini sema neno tu, na roho yangu itapona.

Mwili wa Bwana wetu Yesu Kristo ukulinde, mwili na roho hata uzima wa milele.

Damu ya Bwana wetu Yesu Kristo ikulinde, mwili na roho, hata uzima wa milele.

---

*Kama washiriki ni wengi, zikaimbwe nyimbo, usiimbe wewe wakati wote mpaka kwenda madhabahuni. Bali uache kuimba mapema, sema tena zile sala ulizozisema kwanza:*

Bwana Yesu, ninakuomba, Uje kwangu, unisatishe.

Bwana Yesu, Uje kwangu, unipo-



Kasisi anashirikisha watu.

UKITAKA KUSHIRIKI

nye roho yangu.

Bwana Yesu, uje kwangu unipe nguvu zako.

Bwana Yesu, nakupenda. Uje kwangu, ukae ndani yangu.

Yesu, Bwana wangu na Mungu wangu, uje kwangu ukae ndani yangu.

---

*Baada ya kushiriki ukiisha fika mahali pako, sema sala hizi moyoni, hata mara mbili tatu.*

Bwana Yesu, Mungu wangu, ninakushukuru.

Bwana Yesu, usiniache tena.

Bwana Yesu, unipe nguvu zako.

Bwana Yesu, unishike mkono nisitende dhambi.

Yesu, Wewe ni Bwana wangu na Mungu wangu, nakupenda. Usiniache tena.

*Kama una nafasi sema Sala za kushukuru, uk. 64 wakati washirikipo wengine, hata Kasisi awe tayari kuendelea kusoma Sala za Missa.*



USIPOTAKA KUSHIRIKI

hii ya Mwili na Damu ya Bwana Yesu.

(1) *Ikiwa uimbo unaimbwa, na wewe bado hujamaliza sala hizo uzimalize baada ya uimbo.*

*Tena kama una nafasi, kabla Kasisi hajawa tayari kuendelea kusema Missa, sema sala hizi, hata mara mbili tatu.*

Ee Mungu, Baba, Mwana, Roho Mtakatifu, unitazame, mtoto wako.

Nimekuamini: niwe mwaminifu hata kufa.

Nimekutumaini: kwa kuwa u Baba yangu.

Nakupenda: kwa kuwa Wewe ni Mungu wangu na Mwokozi wangu.

Nimetubu: nimesikitika kwa kuwa nimekukosa.

Sikukosi tena: unijalie nikupendeze hata mwisho.

Mungu, Baba, Mwana, Roho Mtakatifu, unisikie. Kwa Kristo Bwana wetu. Amin.

(*Kasisi aseme kwa siri*).

Utujalie Bwana, tukipokee kwa nia safi tulichopewa kinywani; karama hii tupewayo duniani ituponye hata milele na milele.

Mwili wako nilioupokea, na Damu yako niliyoinywa, iambatane nami, Bwana. Unijalie yasisalie mawaa ya dhambi kwangu, niliyesafika kwa siri zako takatifu, safi. Uishiye na kumiliki milele na milele. Amin.

## AYA YA USHIRIKA.

*Simama.*

*V*. Bwana akae nanyi.
*R*. Akae na roho yako.

Tuombe.

## SALA ZA MWISHO.


*V*. Bwana akae nanyi.
*R*. Akae na roho yako.
*V*. Nendeni zenu kwa amani.
*R*. Tumshukuru Mungu.

*Au.*

*V*. Tumhimidi Bwana.
*R*. Tumshukuru Mungu.



Kasisi anawabariki watu.



Kasisi anasoma Injili ya mwisho.



*Au katika Missa ya Wafu.*

*V.* Wastarehe katika amani.

*R.* Amin.

(*Kasisi aseme kwa siri*).

Ee Utatu Mtakatifu, upende kuikubali ibada yetu : utujalie kwa rehema yako Sadaka hii tuliyoitoa sisi tusiostahili, mbele zako Wewe uliye Mtukufu, itufalie sisi na wote tuliowatolea. Kwa Kristo Bwana wetu. Amin.

[*Askofu aseme kabla ya baraka.*

*V.* Jina la Bwana lihimidiwe.

*R.* Tangu leo na hata milele.

*V.* Msaada wetu u katika Jina la Bwana.

*R.* Aliyezifanya mbingu na nchi.]

BARAKA

*V.* Bwana akae nanyi.

*R.* Akae na roho yako.

✠ Mwanzo wa Injili takatifu kama ilivyoandikwa na Yohana Mt.

*R.* Atukuzwe Bwana.

INJILI YA KAWAIDA

*R.* Tumshukuru Mungu.

## SALA ZA KUSHUKURU

Mwenyezi Mungu, Baba yetu wa mbinguni, nakushukuru.

Nakushukuru kwa kuwa ulimleta Kristo duniani.

Nakushukuru kwa kufa kwake na kwa kufufuka kwake.

Nakushukuru kwa kuwa yumo katika Sakramenti hii; na kwa kuwa amekuja kwangu leo.

Nakushukuru kwa sababu umenipa ruhusa ya kumpokea.

Nakuomba umtazame Kristo, Mwana wako; kwa ajili yake utukubali; utusamehe utubariki sisi na jamaa zetu.

Nakuomba uwabariki Wakristo wote, kila mtu kwa haja yake. Ulibariki Kanisa, lizidi kutakasika. Uwaongoe watu wasio wakristo. Uwastareheshe waliofariki dunia katika imani ya Kikristo.

Bwana Yesu, nakushukuru kwa kuwa umo moyoni mwangu.



Bwana Yesu, nakushukuru kwa kuwa umenisamehe; na kunihurumia.

Bwana Yesu nakushukuru kwa moyo wangu wote.

Bwana Yesu, nakuomba usiniache. Unijaze nguvu zako. Unishike mkono, nisianguke.

Bwana Yesu, nitakufuata tangu leo. Amri zako zote nitazishika. Hatari za dhambi nitaziepuka. Nataka nikutii mpaka kufa.

Bwana Yesu, ukae ndani yangu, unijalie nikukumbuke vema. Ukae nami kila wakati.

Nikutegemee Wewe peke yako.

Mungu Roho Mtakatifu, unikubali, unitawale.

Mungu Roho, nakutolea nafsi yangu, kuwa sadaka kwako.

Mungu Roho, nakupa mawazo yangu yote, nisiwaze mabaya tena.

Nakupa na ulimi wangu, nisiseme mabaya wala kutukana.

Nakupa na mwili wangu wote, nisifanye mabaya wala kulewa.

Mungu Roho, unikubali, unitakase; unipe nguvu za kushinda adui zangu zote; kwa Kristo Bwana wetu. Amin.

Baba yetu.

Salamu, Mariamu.

## ROHO YA KRISTO.

Roho ya Kristo initakase.
Mwili wa Kristo uniponye.
Damu ya Kristo inifurahishe.
Maji ya ubavu wa Kristo yanioshe.
Mateso ya Kristo yanifariji.
Yesu mwema, unisikie.
Ndani ya jeraha zako unifiche.
Usiniache nitengane nawe.
Na yule adui mwovu unilinde.
Saa ya kufa kwangu uniite.
Uniambie nije kwako.
Nikusifu pamoja na Watakatifu wako.
Milele na milele. Amin.



## MWENYEZI MUNGU AHIMIDIWE.

Mwenyezi Mungu ahimidiwe.

Jina lake takatifu lihimidiwe.

Yesu Kristo, Mungu kweli na Mwana-damu kweli, ahimidiwe.

Jina takatifu la Yesu lihimidiwe.

Moyo wake mtakatifu uhimidiwe,

Yesu Kristo, aliemo katika Sakramenti Takatifu, ahimidiwe.

Roho Mtakatifu, Mfariji, ahimidiwe.

Mama wa Mungu, Mariamu Mtakatifu, asifiwe.

Jina la Mariamu, Bikira na Mama, lisifiwe.

Ahimidiwe Mungu kwa ajili ya Malaika zake na Watakatifu wake. Amin.

## Sakramenti ya Toba.

Kuungama dhambi zetu, maana yake nini? Faida yake nini?

Siyo kupata ruhusa ya Ushirika Mt.

Siyo desturi ya dini tu. Hasha!

Kuungama dhambi ndiyo kuomba radhi kwa Mwenyezi Mungu, kwa uradhi alioufanya Bwana Kristo msalabani.

### (1) WEWE HUTAKI KUOMBA RADHI?

Huna hata dhambi? Huna hata kosa? Unayo dhambi. Unalo kosa.

Basi ukifa je! na dhambi bado hujaziungama, utakuwaje?

Wadhani Mungu husahau dhambi tusizotubia? Hazisahau.

Dhambi usizotubia utazikuta kitini pa hukumu ya Mungu, zikakushinda.

Hapana budi una haja kubwa ya kuomba radhi kwa Mungu kila wakati.



### (2) UTAUNGAMA NINI BASI?

Utaungama kila kosa usilotaka kulisikia saa ya kufa kwako, wala siku ya kuhukumiwa.

Ukificha kosa lako unaongeza kosa juu ya kosa.

### (3) JINSI YA KUUNGAMA KWAKO

Ungama kila kosa
kwa jina lake,
kwa namna yake,
kwa mara zake.

Kama hivi:—

Ikiwa umeiba, usiungame "Nimeiba" tu. La! sema hivi:—

Nimeiba *kitu fulani* (ikiwa fedha, nguo, chakula, n.k.)

*Kadiri ya mara* (mara moja, mara tano, mara kumi).

Maana usiloungama halifutiki. Kadhalika kwa kila namna ya dhambi. Ungama jina lake, namna yake, na mara zake.

Hivi wajua kama yote yamefutika na kusamehewa.

Basi kazi ya kwanza ni kujitafuta vema, hata uyafahamu makosa yako, kwa majina yake, namna yake, na kiasi cha mara zake.

## (4) JITAFUTE HIVI

*Piga magoti nyumbani, au Kanisani pasipo sala ya watu, useme na Bwana Kristo :*

Bwana Yesu, ulipenda kufa katika msalaba kwa ajili ya dhambi zangu.

Bwana Yesu, unipe Roho yako Mtakatifu, anikumbushe dhambi zangu nilizozitenda tangu kuungama kwangu mwezi wa ... ... ... (*Taja mwezi*).

Bwana Yesu, unisaidie kuzikumbuka zote, kuzitubia vema, na kuziungama kwa kweli.

### Mawazo.

Nimewaza mambo ya Kiburi ?
Chuki ?
Uchungu ?



Hasira ?
Uwivu ?
Tamaa za dunia ?
Tamaa za mwili ?
Nimetamani fedha au nguo kuliko haki ?

### Maneno.

Nimetukana ?
Nimesema matusi ?
Nimesema machafu ?
Nimesema uwongo ?
Nimeshuhudia uwongo ?
Nimesingizia watu ?

### Matendo.

Nimeiba ? nimeiba nini
Nimepiga watu ?
Nimeingia mambo ya Shetani ?
Nimeshirikiana na Walungu ?
Nimetumia dawa za Shetani ?
Nimetumia Kago ?
Nimeingia ngoma za Shetani ?
Nimetazama ngoma za Shetani ?

Nimekubali kutiwa maji ya Kiislamu nipate dawa?

Nimepiga bao?

Nimevaa hirizi au kumvika mwenzangu nazo?

Nimecheza ngoma mbaya?

Nimetazama ngoma mbaya?

Nimelewa? mara ngapi?

Nimetenda asharati? uzinzi? machafu?

Nimekula kwa ulafi?

Nimefanya udugu nao walioharimishwa?

Nimekuonea haya mbele ya watu?

Nimeuficha ukristo wangu?

## Kutokufanya yanipasayo.

Nimesahau kusali nyumbani?

Nimepunguza sala zangu?

Nimesali bila kufikiri?

Nimekuwa mvivu wa kusali Sala Fupi na Mwalimu?

Nimekosa kusali na mwenzangu nyumbani?

Nimekosa kuihudhuria Missa Siku ya Bwana au Siku za Faradhi? mara ngapi?

Nimekosa Kuungama? tokea lini?



Nimelegea katika Ushirika wangu?

Nimekosa kutoa Sadaka inipasavyo, ndiyo sehemu ya kumi?

Nimekosa kumwangalia au kumwombea mtoto niliyemdhaminia?

Nimekosa Kufunga Siku za Kufunga? mara ngapi?

Nimekosa kujinyima nyama Siku ya Ijumaa? Ijumaa ngapi?

## Kisha, sema mara mbili, tatu.

Ee Bwana Yesu, mabaya haya yote nimeyatenda mimi,
nimekutenda dhambi hizi zote,
nimekuumiza kwa dhambi zangu;
ninakuomba, unisamehe.

## Sala ya Masikitiko.

Ee Mungu, Baba, Mwana, Roho Mtakatifu,
ninasikitika, kwa kuwa nimekutenda dhambi,

ninasikitika, kwa kuwa nimekuasi
 Wewe, Baba yangu,
ninasikitika, kwa kuwa nimekuhuzunisha Wewe, Mwokozi wangu,
ninasikitika, kwa kuwa nimekudharau
 Wewe, Roho wa utakaso.

Bwana Yesu, ninasikitika, sana,
 ninasikitika, kwa kuwa nimekuumzia,
 ninasikitika, kwa kuwa nimedharau
 Damu yako ya thamani.

Ee Mungu, tokea sasa sitaki kutenda dhambi tena.

Ee Mungu, ninaziacha dhambi zangu.

Ee Mungu, nakupenda; unijalie nikupendeze.

Bwana Yesu, unisamehe.

Bwana Yesu, unipe nguvu, nisikose tena.

Bwana Yesu, unishike mkono, nisitende dhambi.

Ee Roho Mtakatifu, unisaidie kuziungama vema dhambi zangu zote, kwa utukufu wa Baba yangu wa mbinguni. Kwa Kristo Bwana wetu. Amin.



## Ufikapo Kanisani.

Sema tena sala hizi ulizozisema baada ya kujitafutia, ukianza "Ee Bwana Yesu, mabaya haya yote........" hata mwisho.

*Ni heri kuzisema mara mbili, tatu, au zaidi, ikiwa watu ni wengi, unakawia kupata nafasi ya kuungama.*

*La! hazitoshi sala hizi, yafaa kusoma Zaburi, kama* 6, 32, 38, 51, 102, 130, 143.

## Ufikapo Penye Maungamo.

(1) Isikilize baraka aitoayo Kasisi.

(2) Sema:

Naungama kwa Mwenyezi Mungu, kwa Watakatifu wote, na kwako, baba, ya kwamba nimekosa sana, kwa mawazo, na maneno, na matendo; kwa kosa langu, kosa langu, kosa langu baya sana. Na tangu nilipoungama na kupata ghofira, (*Taja muda gani uliopita tangu ungamo lako la mwisho. Ikiwa hukupata ghofira, umweleze Kasisi.*) dhambi zangu ninazofahamu

ndizo hizi :—

[HAPO TAJA KILA DHAMBI
JINA LAKE
NAMNA YAKE
MARA ZAKE

Ukiisha, sema]

Kwa dhambi hizi, na nyinginezo nisizozifahamu, nasikitika sana ; nataka kuziacha ; naomba ghofira kwa Mungu, na kwako, baba, nataka kitubio.

(3) Umsikilize vema Kasisi wako.
Pokea mashauri yake.
Fuata maonyo yake.
Timiza kitubio cho chote unachoamriwa naye.

(4) Kasisi akianza kusema maneno ya ghofira, uyapokee kwa unyenyekevu na shukrani ; kadhalika na Baraka.

*Neno la ghofira hasa ni :*

Nakughofiri dhambi zako zote, kwa Jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu. Amin.



## Ufikapo Mahali Pako Tena.

(1) Kwanza ukitimize Kitubio ulichoamriwa, ikiwezekana kukitimiza Kanisani. Kama hukitimizi, kwa uvivu na kwa ukaidi, ghofira yako haikufai.

(2) Umtolee Mungu shukrani, useme sala hizi, hata mara mbili, tatu :

Ee Baba wa upendo, ninakushukuru,
umenifanyia huruma nyingi ; umenipa, mwana wako, ukombozi wa dhambi zangu ; umenijalia ghofira leo hivi.
Ee Baba wa upendo, ninakushukuru.

Ee Roho Mtakatifu, ninakushukuru,
umenitakasa tokea ubatizo wangu ; umenisamehe yote niliyokukosa ; umenitakasa tena kwa ghofira hii ya leo.
Ee Roho Mtakatifu, ninakushukuru.

Ee Bwana Yesu, ninakushukuru kwa pendo lako na kwa kuzaliwa kwako.
Ninakushukuru kwa huruma zako na kwa mateso yako.

Ninakushukuru kwa kufa kwako na kwa Damu yako ya thamani.

Ee Bwana Yesu, ninakushukuru kwa kunipa ghofira leo.

Ninakushukuru kwa kunisamehe dhambi zangu.

Ninakushukuru kwa kuwa nimepatanishwa na Mungu, na watu wote wa Kanisa.

Ee Bwana Yesu, usiniache nitengane nawe;
usiniache nianguke tena;
usiniache nishindwe na Shetani.

Ee Bwana Yesu, unijalie nikupende;
unijalie nikusikilize;
unijalie nikae karibu yako.

Ee Bwana Yesu, Damu yako inilinde na majaribu;
Damu yako iniepushe na dhambi;
Damu yako inisafishe moyo wangu.

Utukufu.

Baba yetu.

Salamu, Mariamu.



*Ukipenda kuongeza sala, chagua katika hizi:*

Roho ya Kristo initakase. (*uk.* 66).

Mwenyezi Mungu ahimidiwe. (*uk.* 67).

Zaburi zifaazo ndizo hizi:

23, 25, 26, 27, 32, 33, 34.

## Sala Fupi za Moyoni.

*Hizi zatufaa tuzijue kuzisema kimoyomoyo, kila sala kwa wakati wake.*

(*1*) *Wakati wa kujaribiwa, hata majaribu yapite.*

Bwana Yesu, unishike mkono, nisitende dhambi.

Bwana Mungu, umo ndani yangu, uniokoe.

Mungu, unanipenda, niokoe na dhambi hii.

(*2*) *Majaribu yakiisha pita.*

Mungu, ninakushukuru.

Bwana Yesu, ninakushukuru.

*(3) Kabla ya kazi na mwisho wake.*

Baba, uibariki kazi yangu na kuikubali.

*(4) Ukiisha ona kuwa umekosa.*

Mungu, Baba, unisamehe.

Bwana Yesu, unisamehe.

*(5) Ukiwa unakwenda kwa* fulani, *au* fulani *anakuja kwako.*

Ee Baba, utubariki mimi na *fulani*, tukupendeze kwa vyote.

*(6) Wakati wo wote, nyumbani, shambani, njiani.*

Mungu wangu, nakupenda.
Mungu, unanipenda, nimejiweka kwako.
Bwana Yesu, unifunge kwako.
Upendo, najiweka kwako ;
Tokea sasa, mimi wako.

*Wakati wo wote, mahali po pote, yafaa kusema,*

Baba yetu.
Salamu, Mariamu.
Roho ya Kristo initakase. (*uk.* 66).
Mwenyezi Mungu ahimidiwe. (*uk.* 67).

## Kukibariki Chakula.

### *Kabla ya kula.*

✠ Unibariki, Mungu wangu, ukibariki na chakula changu, nipate nguvu kukutumikia vema. Amin.

### *Baada ya kula.*

✠ Ninakushukuru, Mungu wangu kwa chakula hiki, na kwa baraka zako zote. Amin.

# Ibada ya Baraka ya Sakramenti Mbarikiwa.

*Watu wakionapo Kijumba cha Sakramenti kimefunguliwa, na waimbe,*

Dhabihu ya wokovu wetu,
Umetufungulia mbingu;
Adui watusonga sana,
Kwa nguvu utusaidie.

Ee Mungu mmoja, Nafsi tatu,
Twakutukuza sikuzote:
Utupe raha ya milele
Katika nchi yetu juu. Amin.

*Wimbo huu ukimalizika, Kasisi aagize* Litania *au* Wimbo *mwingine ulioruhusiwa kwa Ibada hii, au* Te Deum (*uk. 90*), *au zisemwe sala zifaazo.*

*Kisha watu waimbe.*

Siri hii iliyo kubwa
Tuisujudie vema,
Ya zamani yamepita,
Mambo ya Torati ile;
Na yasiyoonekana
Tunaona kwa imani.



Utukufu na fahari
Ina Mungu juu ya yote,
Baba, Mwana, naye Roho,
Nafsi tatu, Mungu mmoja;
Atukuzwe, asifiwe,
Leo, kesho, na milele. Amin.

*Kisha Kantor aimbe,*

*V.* Uliwapa chakula cha mbinguni. (Haleluya.)
*R.* Ndicho kilicho kitamu. (Haleluya)

(Halleluya *isiimbwe ila Wakati wa Pasaka na Sikukuu ya Mwili Mt.*)

*Kasisi asimame, akaimbe,*

Tuombe.

Ee Mungu, umetuachia ukumbusho wa Mateso yako, katika Sakramenti iliyo ya ajabu: Utujalie, tunakusihi, tuziheshimu siri takatifu za Mwili na Damu yako; ili tuyaone daima ndani yetu mazao ya ukombozi wako. Uishiye na kumiliki pamoja na Mungu Baba, katika umoja wa Roho Mtakatifu, Mungu, daima milele na milele. *Amin.*

*Ndipo hutolewa Baraka.*

*Mara Kasisi ameondolewa veli ya mabegani, watu waseme baada yake fungu kwa fungu,*

Mwenyezi Mungu ahimidiwe.
Jina lake takatifu lihimidiwe.
Yesu Kristo, Mungu kweli na Mwanadamu kweli, ahimidiwe.

Jina takatifu la Yesu lihimidiwe.

Moyo wake mtakatifu uhimidiwe.

Yesu Kristo, aliomo katika Sakramenti Takatifu, ahimidiwe.

Roho Mtakatifu, Mfariji, ahimidiwe.

Mama wa Mungu, Mariamu Mtakatifu, asifiwe.

Jina la Mariamu, Bikira na Mama, lisifiwe.

Ahimidiwe Mungu kwa ajili ya Malaika zake na Watakatifu wake. Amin.

*Kisha Sakramenti ifunikwe tena, huko nyuma watu waimbe,*

*Ant.* Tuiabudu Sakramenti Takatifu : milele na milele.

*Zab.* 117.

1. Msifuni Bwana, enyi mataifa yote : mhimidini, enyi watu wote.

2. Maana fadhili zake kwetu sisi ni kuu : na uaminifu wa Bwana ni wa milele.

Utukufu una Baba na Mwana : na Roho Mtakatifu.

Ulivyokuwa mwanzo : ulivyo sasa, utakavyokuwa milele. Amin.

*Ant.* Tuiabudu Sakramenti Takatifu : milele na milele.

# Jinsi ya Kusali mbele za Bwana Yesu Katika Sakramenti Mb.

*Piga magoti mbele ya Kijumba cha Sakramenti Mb.*

✠ Kwa Jina la Baba na Mwana na Roho Mtakatifu. *Amin.*

Baba yetu.

Salamu, Mariamu.

*Sema kwa taratibu sana, moyoni,*

Mungu wangu, wanipenda ; ninakushukuru.

Mungu wangu, umefanyika Mwanadamu ; ninakusifu.

Mungu wangu, ulikufa kwa ajili yangu ; ninakutukuza.

Mungu wangu, umo katika Sakramenti hii ; ninakuabudu.

Yesu, Mungu wangu, ninakushukuru.

Yesu, Mungu wangu, ninakusifu.

Yesu, Mungu wangu, ninakuabudu.

Utatu Mtukufu, Mungu wangu, ninakutukuza.

Utatu Mtukufu, Mungu wangu, ninakuhimidi.

Utatu Mtukufu, Mungu wangu, ninakusifu.

Utatu Mtukufu, Mungu wangu, ninakushukuru.

Mungu Baba, Upendo, Yesu ni wako; nami ni wako ndani yake.

Mungu Baba, Upendo, Yesu ni sadaka kwako; nami ninajitoa sadaka kwako ndani yake.

Mungu Baba, Upendo, Yesu ndiye akupendezaye; unijalie nikupendeze ndani yake.

Yesu, Mwokozi, nimekutenda dhambi.

Yesu, Mwokozi, unisamehe.

Yesu, Mwokozi, unisafishe roho.

Bwana Yesu, unishike mkono, nisizidi kutenda dhambi.

Bwana Yesu, naomba Kanisa lako lizidi kuongezeka.

Bwana Yesu, naomba wote wakugeukie.

Bwana Yesu, naomba wasikiaji wako wakuangukie.

Bwana Yesu, naomba wanafunzi wako watiliwe nuru.

Bwana Yesu, naomba wakristo wote watakaswe.

Bwana Yesu, naomba Askofu wangu abarikiwe nawe.

Bwana Yesu, naomba makasisi wote wapewe baraka yako.

Bwana Yesu, naomba waalimu wa dini wasaidiwe nawe.

Bwana Yesu, naomba kila kazi ya Kanisa mtaani mwetu ifanikishwe nawe.



Bwana Yesu, naomba wagonjwa waponywe na kufarijika.

Bwana Yesu, naomba waliofariki katika imani wazidi kustarehe kwako.

Bwana Yesu, naomba unifunulie yanipasayo katika dini yako,

nikione Bwana wa wote na Mwokozi wao,
nipendane na ndugu zangu, watoto wako,
niwasamehe adui zangu,
niwahudumie jirani zangu,
niwapende ndugu zangu kama nafsi yangu.

Bwana Yesu, haya yote niyaombayo ndiyo uyapendayo Wewe. Basi na yawepo, Bwana.

Uyalete kwa uweza wako.

Yote yawezekana kwako, Bwana.

Bwana Yesu, ninaomba kwako haja zangu hizi;

nyumba yangu, na wote waliomo humo, uwabariki sana;
mwenzangu nipendane naye na kumheshimu;
watoto wangu niwalee kwa adabu za Kikristo;
wazee wangu niwaheshimu na kuwasaidia;
jamaa zangu zote wakugeukie, na kutakaswa;
mashamba yetu yasitawi.

Bwana Yesu, ninajitoa kwako kuwa sadaka, ninajiweka kwako tokea sasa.

Bwana Yesu, unijalie kuwaza yaliyo mazuri, safi,
Unijalie kusema yaliyo safi na ya amani tu.
Unijalie nisitende mabaya yo yote.

Bwana Yesu, mimi si kitu,
wala sina kitu,
wala sitaki kitu, ila Wewe.

Bwana Yesu, ninakushukuru.

Bwana Yesu, nakwenda zangu kwenye majaribu;
ukae ndani yangu,
usiniache nitengane nawe,
unishike mkono, nisitende dhambi.

Baba yetu.

Roho ya Kristo initakase.

Mwenyezi Mungu ahimidiwe.

*Kama una nafasi bado, sema wimbo 181.*

✠ Roho zao waaminifu kwa rehema ya Mungu wastarehe katika amani. *Amin.*

## Siku zenye Missa ya faradhi kwa wote.

1. Kila Siku ya Bwana mwaka mzima.
2. Sikukuu ya Kuzaliwa Bwana (*Des. 25*).
3. Ufunuo wa Bwana (*Jan. 6*).
4. Kupaa kwa Bwana.
5. Mwili Mtukufu wa Bwana, (*lakini ni halali kuiadhimisha Sikukuu hii Siku ya Bwana ifuatayo*).
6. Kustarehe kwa Mariamu Bikira Mbarikiwa (*Agosti 15*).
7. Sikukuu ya Watakatifu wote (*Nov. 1*),

SIKU HIZO KILA MKRISTO AIHUDHURIE MISSA.

# Te Deum.

1. Wewe, Mungu, twakusifu: Wewe, Baba, twakukiri,
2. Wewe Baba wa milele: ulimwengu wote unakuabudu.
3. Wewe Malaika zote: nazo Mbingu na Nguvu zote.
4. Nao Makerubi na Maserafi: wakuimbia hawakomi.
5. Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu: Bwana Mungu wa majeshi.
6. Mbingu na nchi zimejaa: enzi ya utukufu wako.

7. Wakusifu Wewe: jamii tukufu ya Mitume.
8. Wakusifu Wewe: shirika lenye sifa la Manabii.
9. Wakusifu Wewe: jeshi la Mashahidi waliovaa mavazi meupe.
10. Kanisa takatifu katika nchi zote: lakukiri Wewe.
11. Baba mwenye enzi: isiyo na kiasi.
12. Mwana wako pekee: wa kweli, wa kuabudiwa.
13. Na Mfariji: Roho Mtakatifu.

14. Wewe Kristo: ndiwe Mfalme wa Utukufu.
15. Wewe Mwana wa milele: wa Baba.



16. Wewe ulipotaka kujifanya mtu, ili umwokoe mwanadamu: hukuchukizwa na tumbo lake Bikira.
17. Wewe ulipoushinda uchungu wa mauti: uliwafungulia waaminio Ufalme wa Mbinguni.
18. Wewe unakaa mkono wa kuume wa Mungu: katika utukufu wake Baba.
19. Tunasadiki utakuja: kuwa Mwamuzi.
(*Piga magoti*).
20. Kwa hiyo twakuomba, uwasaidie watumwa wako: uliowakomboa kwa damu yako ya thamani.
(*Simama*).
21. Uwajalie pamoja na Watakatifu wako: utukufu wa milele.

22. Uwaokoe watu wako, Bwana: uubariki urithi wako.
23. Uwatawale: uwainue hata makao ya milele.
24. Sisi kila siku: twakutukuza.
25. Twalisifu Jina lako: zamani hizi na za milele.
26. Ukubali, Bwana, kutulinda: leo tusitende dhambi
27. Uturehemu, Bwana: uturehemu sisi.
28. Utuonee huruma, Bwana: kwa kuwa twakutumaini Wewe.
29. Nimekutumaini Wewe, Bwana: nisipotee milele.

NYARAKA NA INJILI ZA SIKU ZA BWANA NA SIKU NYINGINEZO.

| Siku | Waraka | Injili |
|---|---|---|
| I Majilio | Warumi 13: 11-14 | Luka 21: 25-33 |
| II Majilio | Warumi 15: 4-13 | Matt. 11: 2-10 |
| III Majilio | Wafilipi 4: 4-7 | Yoh. 1: 19-28 |
| IV Majilio | 1 Wakor. 4: 1-5 | Luka 3: 1-6 |
| Mkesha wa Kuzaliwa Bwana | Warumi 1: 1-6 | Matt, 1: 18-21 |
| Kuzaliwa Bwana | | |
| Missa ya I | Tito 2: 11-15 | Luka 2: 1-14 |
| Missa ya II | Tito 3: 4-7 | Luka 2: 15-20 |
| Missa ya III | Waebr. 1: 1-12 | Yoh. 1: 1-14 |
| Stefano Sh. | Mate. 7: 55-60 | Matt. 23: 34-39 |
| Yohana Mtu. | 1 Yoh. 1: 1-10 | Yoh. 21: 19-24 |
| Wasio Hatia | Ufunuo 14: 1-5 | Matt. 2: 13-18 |
| S.B. katika Okt. ya Kuzaliwa | Wagalatia 4: 1-7 | Luka 2: 33-40 |



| Siku | Waraka | Injili |
|---|---|---|
| Kutahiriwa Bwana | Tito 2: 11-15 | Luka 2 21 |
| Mkesha wa Ufunuo | Wagal. 4: 1-7 | Matt. 2: 19-23 |
| Ufunuo wa Bwana | Isaya 60: 1-6 | Matt. 2: 1-12 |
| I Ufunuo | Warumi 12: 1-5 | Luka 2: 42-52 |
| S. 8 ya Ufunuo | Isaya 60: 1-6 | Yoh. 1: 29-34 |
| II Ufunuo | Warumi 12: 6-16 | Yoh. 2: 1-11 |
| III Ufunuo | Warumi 12: 16-21 | Matt. 8: 1-13 |
| IV Ufunuo | Warumi 13: 8-10 | Matt. 8: 23-27 |
| V Ufunuo | Wakol. 3: 12-17 | Matt. 13: 24-30 |
| VI Ufunuo | I Wathes. 1: 2-10 | Matt. 13: 31-35 |
| Septuajesima | I Wakor. 9: 24-10: 5 | Matt. 20: 1-16 |
| Seksajesima | II Wakor. 11: 19-12: 9 | Luka 8: 4-15 |
| Kwinkwajesima | I Wakor. 13: 1-13 | Luka 18: 31-43 |

| Siku | Waraka | Injili |
|---|---|---|
| J. 5 ya Majivu | Yoel 2: 12-19 | Matt. 6: 16-21 |
| I Kwaresima | II Wakor. 6: 1-10 | Matt. 4: 1-11 |
| II Kwaresima | I Wathes. 4: 1-7 | Matt. 17: 1-9 |
| III Kwaresima | Waefeso 5: 1-9 | Luka 11: 14-28 |
| IV Kwaresima | Wagal. 4: 22-31 | Yoh. 6: 1-15 |
| S.B. ya Mateso | Waebr. 9: 11-15 | Yoh. 8: 46-59 |
| S.B. ya Mitende | Wafil. 2: 5-11 | Matt. 26: 1-27: 66 |
| J. 3 Katika Juma Takatifu | Isaya 50: 5-10 | Yoh. 12: 1-9 |
| J. 4 Katika Juma Takatifu | Yere. 11: 18-20 | Marko 14: 1-15: 46 |
| J. 5 Katika Juma Takatifu | [1] Isaya 62: 11-63: 7 | |
| | [2] Isaya 53: 1-12 | Luka 22: 1-23: 53 |



| Siku | Waraka | Injili |
|---|---|---|
| Alh. ya Amri | I Wakor. 11: 20-32 | Yoh. 13 1-15 |
| Ijumaa Kuu | Waebr. 10: 1-25 | Yoh. 18: 1-19: 42 |
| Mkesha wa Pasaka | Wakol. 3: 1-4 | Matt. 28: 1-7 |
| Pasaka | I Wakor. 5: 7-8 | Marko 16: 1-7 |
| J. 3 ya Pasaka | Mate 10: 34-43 | Luka 24: 13-35 |
| J. 4 ya Pasaka | Mate. 13: 26-32 | Luka 24: 36-47 |
| J. 5 ya Pasaka | Mate. 3: 13-19 | Yoh. 21: 1-14 |
| Alh. ya Pasaka | Mate. 8: 26-40 | Yoh. 20: 11-18 |
| Ij. ya Pasaka | I Petro 3: 18-22 | Matt. 28: 16-20 |
| J. 1 ya Pasaka | I Petro 2: 1-10 | Yoh. 20: 1-9 |

| Siku | Waraka | Injili |
|---|---|---|
| I Pasaka | I Yoh. 5: 4-10 | Yoh. 20: 19-31 |
| II Pasaka | I Petro 2: 21-25 | Yoh. 10: 11-16 |
| III Pasaka | I Petro 2: 11-19 | Yoh. 16: 16-22 |
| IV Pasaka | Yakobo 1: 17-21 | Yoh. 16: 5-14 |
| V Pasaka | Yakobo 1: 22-27 | Yoh. 16: 23-30 |
| Mkesha wa Kupaa | Waef. 4: 7-13 | Yoh. 17: 1-11 |
| Kupaa | Matendo 1: 1-11 | Marko 16: 14-20 |
| S.B. katika Oktavo ya Kupaa | I Petro 4: 7-11 | Yoh. 15: 26-16: 4 |
| Mkesha wa Pentekote | Mate. 19: 1-8 | Yoh. 14: 15-21 |
| Pentekote | Matendo 2: 1-11 | Yoh. 14: 23-31 |
| J. 3 ya Pentekote | Mate. 10: 42-48 | Yoh. 3: 16-21 |
| J. 4 ya Pentekote | Mate. 8: 14-17 | Yoh. 10: 1-10 |



| Siku | Waraka | Injili |
|---|---|---|
| J. 5 ya Pentekote | Mate. 5: 12-16 | Yoh. 6: 44-51 |
| Alh. ya Pentekote | Mate. 8: 5-8 | Luka 9: 1-6 |
| Ij. ya Pentekote | Yoel 2: 23-27 | Luka 5: 17-26 |
| J. 1 ya Pentekote | Warumi 5: 1-5 | Luka 4: 38-44 |
| Utatu Mtukufu | Warumi 11: 33-36 | Matt. 28: 18-20 |
| Mwili Mtukufu | I Wakor. 11: 23-29 | Yoh. 6: 55-58 |
| S.B. katika Oktavo ya Mwili Mtukufu, (II Pente). | I Yoh. 3: 13-18 | Luka 14: 16-24 |
| Moyo Mtakatifu | Isaya 12: 1-6 | Yoh. 19: 31-35 |
| III Pentekote | I Petro 5: 6-11 | Luka 15: 1-10 |
| IV Pentekote | Warumi 8: 18-23 | Luka 5: 1-11 |
| V Pentekote | I Petro 3: 8-15 | Matt. 5: 20-24 |

| Siku | Waraka | Injili |
|---|---|---|
| VI Pentekote | | |
| | Warumi 6: 3-11 | Marko 8: 1-9 |
| VII Pentekote | | |
| | Warumi 6: 19-23 | Matt. 7: 15-21 |
| VIII Pentekote | | |
| | Warumi 8: 12-17 | Luka 16: 1-9 |
| IX Pentekote | | |
| | I Wakor. 10: 6-13 | Luka 19: 41-47 |
| X Pentekote | | |
| | I Wakor. 12: 2-11 | Luka 18: 9-14 |
| XI Pentekote | | |
| | I Wakor. 15: 1-10 | Marko 7: 31-37 |
| XII Pentekote | | |
| | II Wakor. 3: 4-10 | Luka 10: 23-37 |
| XIII Pentekote | | |
| | Wagal. 3: 16-22 | Luka 17: 11-19 |
| XIV Pentekote | | |
| | Wagal. 5: 16-24 | Matt. 6: 24-33 |
| XV Pentekote | | |
| | Wagal. 5: 25-6: 10 | Luka 7: 11-16 |
| XVI Pentekote | | |
| | Waef. 3: 13-21 | Luka 14: 1-11 |
| XVII Pentekote | | |
| | Waef. 4: 1-6 | Matt. 22: 35-46 |



| Siku | Waraka | Injili |
|---|---|---|
| XVIII Pentekote | | |
| | I Wakor. 1; 4-8 | Matt. 9: 1-8 |
| XIX Pentekote | | |
| | Waef. 4: 23-28 | Matt. 22: 2-14 |
| XX Pentekote | | |
| | Waef. 5: 15-21 | Yoh. 4; 46-53 |
| XXI Pentekote | | |
| | Waef. 6: 10-17 | Matt. 18: 21-35 |
| XXII Pentekote | | |
| | Wafil. 1: 3-11 | Matt. 22: 15-21 |
| XXIII Pentekote | | |
| | Wafil. 3: 17-4: 3 | Matt. 9: 18-26 |
| XXIV Pentekote | | |
| | Wakol. 1: 9-14 | Matt. 24: 15-35 |
| Andrea Mtu. *(Nov. 30)* | | |
| | Warumi 10: 10-18 | Matt. 4: 18-22 |
| Kuchukuliwa mimba Mariamu B. Mb. *(Des. 8)* | | |
| | Isaya 7: 10-15 | Luka 1: 26-28 |
| Tomaso Mtume, *(Des. 21)* | | |
| | Waef. 2: 19-22 | Yoh. 20: 24-29 |
| Kuongoka Paolo Mtu. *(Jan. 25)* | | |
| | Mate. 9: 1-12 | Matt 19: 27-29 |

| Siku | Waraka | Injili |
|---|---|---|
| Kutakaswa Mariamu, B. Mb. (*Feb.* 2) | Malaki 3: 1-4 | Luka 2: 22-32 |
| Mattiya Mtu. (*Feb.* 24, *au* 25) | Mate. 1: 15-26 | Matt. 11: 25-30 |
| Kuhubiriwa Mariamu Mb. (*Mar.* 25) | Isaya 7: 10-15 | Luka 1: 26-38 |
| Marko Mtunga Injili (*Apr.* 25) | Ezekieli 1: 10-14 | Luka 10: 1-9 |
| Yusuf Mt. (*J. 5 ifuatayo S.B. II Pasaka*) | Mwanzo 49: 22-26 | Luka 3: 21-23 |
| Filipo na Yakobo, Mitume (*Mei* 1.) | Hekima 5: 1-5 | Yoh. 14: 1-13 |
| Barnaba Mtume (*Juni* 11.) | Mate. 11: 21-26 na 13: 1-3 | Matt. 10; 16-22 |
| Kuzaliwa Yohana Mbatizaji (*Juni* 24.) | Isaya 49: 1-7 | Luka 1; 57-68 |
| Petro na Paolo Mit. (*Juni* 29.) | Mate. 12: 1-11 | Matt. 16: 13-19 |
| Damu iliyo ya thamani ya Bwana (*Julai* 1) | Waebr. 9: 11-15 | Yoh. 19: 30-35 |
| Kusalimiwa Elizabeti na Mariamu Mb. (*Julai* 2.) | Isaya 7: 10-15 | Luka 1: 39-47 |
| Yakobo Mtu. (*Julai* 25.) | I Wakor 4: 9-15 | Matt. 20: 20-23 |



| Siku | Waraka | Injili |
|---|---|---|
| Kung'aa kwa Bwana (*Agosti* 6.) | II Petro 1: 16-19 | Matt. 17: 1-9 |
| Jina Takatifu, Yesu (*Agosti* 7.) | Mate. 4: 8-21 | Luka 2: 21 |
| Kustarehe Mariamu Mb. (*Agosti* 15) | Yoshua bin Sirak 24: 11-20 | Luka 10: 38-42 |
| Bartolomayo Mtu. *Agosti* 24.) | I Wakor. 12: 27-30 | Luka 6: 12-19 |
| Kuzaliwa Mariamu Mb. (*Sept.* 8.) | Isaya 7: 10-15 | Luka 1: 26-28 |
| Msalaba Mtakatifu (*Sept.* 14.) | Wafilipi 2: 5-11 | Yoh. 12: 31-46 |
| Mattayo Mtume (*Sept.* 21) | Ezekieli 1: 10-14 | Matt. 9: 9-13 |
| Mikael na Malaika zote (*Sept.* 29.) | Ufunuo 1: 1-5 | Matt. 18: 1-10 |
| Luka Mtunga Injili (*Okt.* 18.) | II Wakor. 8: 16-24 | Luka 10: 1-9 |
| Simon na Yuda Mitume (*Okt.* 28.) | Waefeso 4: 7-13 | Yoh. 15: 17-25 |
| Watakatifu wote (*Nov.* 1.) | Ufunuo 7: 2-12 | Matt. 5: 1-12 |